Haki za Binadamu katika British Columbia:
Ulinzi katika ajira

Karatasi hii ya ukweli imetengenezwa ili kukusaidia kuelewa haki za binadamu katika British Columbia na ulinzi unaopata katika ajira.

British Columbia ina sheria ya kulinda na kukuza haki za binadamu. Hii inaitwa *BC Human Rights Code* au *Code (kanuni).* Ikiwa una maswali yoyote tafadhali wasiliana na BC **Human Right Clinic (Kilinki ya BC ya Haki Za binadamu).** Maelezo zaidi kuhusu mawasiliano yanapatikana mwishoni mwa karatasi hii ya ukweli.

Maelezo kwa Wafanyakazi

Code (Kanuni) inalinda waombaji kazi na wafanyakazi.

Jinsi gani ninalindwa katika ajira?

Unalindwa na *Code (Kanuni)* kutokana na ubaguzi katika kuajiri watu au katika kazi ikiwa ubaguzi umetokana na moja au zaidi ya **sifa za binafsi zinazolindwa**:

- Umbari, rangi, asili, pahali pakuzaliwa
- Maelekeo ya kisiasa
- Dini
- Hali ya ndoa
- Hali ya familia
- Ulemavu wa kimwili au kiakili
- Jinsia (pamoja na ujauzito, aliebadili jinsia)
- Maelekeo ya kingono
- Umri (19 na kuendelea)
- Kutiwa hatiani ya jinai au muhtasari wa hatia isio husiana na ajira

Unaweza kuripoti lalamiko kwenye BC Human Rights Tribunal (mahakama ya BC Human Rights) ikiwa unaamini kwamba umebaguliwa kuhusu ajira

Ubaguzi katika ajiria ni nini?

Code (Kanuni) inalinda masuala yote ya ajira, pamoja na:

- matangazo ya ajira
- mahojiano ya kazi
- kuajiri
- mazingira ya kazi
- kupandishwa vyeo na kufukuzwa kazi
- mafao
- mishahara

Ubaguzi ni kumtendea mtu vibaya au kuwakatalia mafao kwa sababu ya sifa binafsi kama vile dini au ulemavu.

Mifano ya ubaguzi katika ajira:

- Kumfukuza mwanamke kazi kwa sababu ya ujauzito
- kutoa maoni ya ngono kuhusu mtu anavyoonekana, mavazi, au sehemu za mwili
- kukataa kuajiri mtu kwa sababu ana ulemavu wa kimwili au kiakili
- kulipa mwanamke kiwango cha chini kuliko mwanaume japokuwa sifa ya kazi ni moja
- kumlazimisha mfanyakazi kustaafu kwa sababu ya umri wake
- kukataa kurekebisha ratiba ya kazi kwa wenye kufata dini

Nitajuaje kama nina malalamiko ya Haki za Binadamu?

Kuripoti malalamiko kwenye *BC Human Rights Code (Kanuni ya haki za binadamu BC)* kuhusu maajira, **yote yafuatayo** lazima yawe ya kweli:

- ✓ umetendewa ubaya
- ✓ Umetendewa tafauti na pia vibaya kwa sababu ya sifa za binafsi, kama vile umbari wako, rangi imani ya dini, jinsia, ulemavu wa kimwili au kiakili, au mwelekeo wa kingono.
- ✓ tendo hilo limetokea kazini au inahusiana na kazi.

Lazima uripoti malalamiko yako katika muda wa miezi sita ya tukio kutokea. (Kumbuka: kuna baadhi ya kesi za kipekee zisizo fuata muda huo uliyowekwa.) Kuripoti lalamiko kuanzisha mchakato wa kisheria sawa na hatua za mahakama. Mtu mwenye kuripoti malalamiko anaitwa **mlalamikaji**.

Maelezo kwaWaajiri

Code (Kanuni) inalinda waombaji kazi na wafanyakazi. Waajiri lazima wahakikishe kwamba:

- Maamuzi ya kuajiri mtu lazima yazingatie vigezo vinavyo husiana na kazi

- Mazingira ya kazi yasiwe na ubaguzi

Wakati wa kuhoji mwombaji kazi

Kwa muajiri mwenye kuuliza maswali wakati wa mahojiano, kanuni ya ujumla ni:

Uliza maswali yanayohitajika katika kufanya uchaguzi wa kuajiri ulingane na ujuzi, uhodari na kustahili

Wakati wa kutangaza kazi

Code (Kanuni) hairuhusu matangazo ya kazi yaulizie sifa za kibinafsi maalumu zinazo lindwa na Code (Kanuni), isipokuwa kama kuna mahitaji maalumu ya halali ya kazi hiyo. Kwa mfano,mwajiri anaweza kutangaza yakuwa wanahitaji kuajiri wanawake tu kufanya kazi ya kupokea katika makazi ya wanawake walionyanyaswa.

Nini wajibu wa kujumuisha watu wengine?

Waajiri lazima wafanye bidii ya kujumuisha watu wenye sifa tofauti za kibinafsi zinazo lindwa na *Code (Kanuni)*. Hii inaitwa **wajibu wa kujumuisha**. Kujumuisha kutegemea na hali maalum.

Kwa mfano, mwajiri anaweza kuhitajika:

- kumpa mtu mafunzo zaidi
- kurekebisha ratiba ya kazi
- kurekebisha au kununua vifaa
- kubadilisha majukumu ya mfanyakazi

Kama unahitaji muundo au marekebisho kazini, mwaambie mwajiri wako. Mwajiri ana wajibu wa kufanya juhudi ya kutosha ya kutafuta sehemu inayomfaa zaidi mfanyakazi - isipokuwa pale kufanya marekebisho ya mahitaji hayo itasababisha **ugumu usio kuwa** na lazima.

Wapi naweza kupata msaada au maelezo zaidi?

Walalamikaji popote katika jimbo wanaweza kupata maelezo kupitia **BC Human Rights Clinic (Kilinki ya BC ya Haki Za binadamu)**. Watu wa kliniki wanaweza kukusaidia kuelewa *Human Rights Code (Kanuni za Haki za Binadamu)* au kushughulikia malalamiko ya haki za binadamu ya jimbo. Unaweza pia ukafuzu kupata aina tafauti za huduma. Zungumza na mtu yoyote katika kliniki ili uone ikiwa utakubaliwa.

Kilinki ya BC ya Haki Za binadamu

300-1140 West Pender Street, Vancouver, B.C. V6E 4G1
Phone: 604 622-1100 Toll Free: 1 855 685-6222
Fax: 604 685-7611
Online: www.BCHRC.net

Wewe ni **mhojiwa** Ikiwa kuna mtu ameripoti malalamiko juu yako. **Wahojiwa** wote kwenye jimbo na walalamikaji wa eneo la Victoria wanaweza kupata maelezo zaidi kwa kuwasiliana na:

University of Victoria

Law Centre Clinical Law Program
Suite 225 – 850 Burdett Avenue, Victoria, B.C. V8W 1B4
Phone: 250 385-1221 Toll Free: 1 866 385-1221
E-mail: reception@thelawcentre.ca

Unaweza kupata maelezo ya ziada kutoka **BC Human Right Tribunal (Mahakama ya BC ya Haki za Binadamu)**:

Mahakama ya BC ya Haki za Binadamu

Suite 1170 – 605 Robson Street, Vancouver, B.C. V6B 5J3
Phone: 604 775-2000 Toll Free: 1 888 440-8844
TTY (walio kuwa na matatizo ya kusikia): 604 775-2021
Online: www.bchrt.gov.bc.ca

Karatsi hii ya maelezo imekusudiwa kwa madhumuni ya kutoa maelezo kwa ujumla tu. Siyo kwa nia ya kuchukuwa nafasi ya ushauri wa kisheria.